

Makamu wa Rais mstaafu, Dk Mohamed Gharib Bilal (kulia) akimsikiliza Profesa Gelase Mutahaba, Baba wa aliyekuwa Mkurugenzi wa Vipindi na Uzalishaji wa Clouds Media Group, Ruge Mutahaba alipofika nyumbani kwake, Mikocheni, Dar es Salaam jana. (Picha na Fadhili Akida).



## \* Kimeta chaua wawili Kilimanjaro, watano wako hoi \*

**Na Flora Mwakasala,  
Moshi**

**W**ATU wawili wamekufa na wengine watano wamelazwa katika Hospitali ya Rufaa ya KCMC na Kilema wilayani Moshi mkoani Kilimanjaro, baada ya kula nyama inayodaiwa kuwa na vimelea vya ugonjwa wa kimeta.

Aidha, watu 97 wanahofia kupata ugonjwa huo ka-

tika kijiji cha Kilema baada ya kula nyama inayodaiwa kuwa na maambukizi hayo.

Akitoa taarifa katika kikao cha Baraza la Madiani wa Halmashauri ya Moshi, Mganga Mkuu wa halmashauri hiyo, Dk Alex Kazula aliwataka wananchi kuchukua tajadheri dhidi ya ugonjwa huo.

Alisema walipokea taarifa wiki iliypita kuwa kulikuwa na wagonjwa saba katika vijiji vya Lekule, Kondeni, Darajani na Kanji,

ambapo wawili wamefariki dunia, watatu wamelazwa Hospitali ya KCMC na wawili Hospitali ya Kilema.

"Tumechukua sampuli na kupeleka katika sehemu ya utafiti KCMC na kwa sasa tunasubiri majibu, lakini wagonjwa wote walikuwa na viashiria vyote vya ugonjwa wa kimeta, tunasubiri majibu ya maabaraka kuthibitisha," alisema.

Alisema tayari wameanza kuchukua hatua za awali ikiwa ni pamoja na kutoa

dawa kwa watu 97 wanaosadikiwa kula nyama yenye maambukizi na kusimamia mazishi ya watu wote walifariki kwa ugonjwa huo.

Aidha, aliwataka wananchi waepuke kula nyama ambazo hazijapimwa na wataalam wa mifugo.

Daktari wa Mifugo katika halamashauri hiyo, Walter Marandu alisema wamepeleka nakala za matangazo ya kukataza kusafirisha mifugo kwenda sehemu nyingine ili kuepuka kuenea kwa

ugonjwa huo.  
Diwani wa Kahe Mashariki, Kamili Mmbando alisema ni lazima madiwani washirikiane na idara ya afya, watendaji wakata na wenyeviti, kuhakikisha wanatoa elimu kuhusu kijihadhari na ugonjwa huo na kuangalia jinsi ya kuudhibiti.

Hivi karibuni ugonjwa huo uliibuka katika wilaya ya Rombo mkoani hapa na kusababisha vifo vya watu watano na ng'ombe 21.

uongoz baada ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kumvua uanachama kutokana na kutoridhishwa na mwenendo wa uongozi wake, aliokuwa akiutumia kuchoea mgogoro wa chanzo cha maji.

Wengine ni Lucas Mgegela, Mrema Gudu na Charles Makima ambao wote walikamatwa juzi jioni kwenye mkutano wa hadhara, uliofanyika kijijini Lola baada ya mkuu wa mkoa kutembelea eneo lenye mgogoro, huku wananchi wakonesha kuwepo kwa uhaba wa maji kijijini.

Wanaoshikiliwa pia walitajwa kuwa miongoni mwa watu waliowahi kufanya kampeni nyingi za kukwamisha kulindwa kwa chanzo cha maji cha kijiji hicho, ikiwemo kutishia maisha ya Ofisa Tarafa wa Kipembawe, Kassim Kirondomara.

Ofisa huyo alitishiwa alipofanya mkutano wa hadhara kwa ajili ya kutoa elimu juu ya nini kinalengwa katika kulinda chanzo cha maji kilichopo katika kijiji hicho.

Kwenye mkutano huo Kirondomara alisema watu wanofanya shughuli za kilimo na ufugaji kwenye bonde lenye chanzo cha maji, pia waling'oa mawe yaliyowekwa kama alama kwa ajili ya kuonyesha mpaka kati ya chanzo cha maji na enelo linalotumika kwa matumizi ya bian-damu.